# Maelezo Yanayohitajika ili Kuwasilisha Ombi la Ukosefu wa Ajira Katika Jimbo la Maine

Maagizo ya video kwa kila hatua yanaweza kupatikana kwenye YouTube (kwa lugha ya Kiingereza tu)
Kufungua Akaunti yako ya ReEmployME: https://www.youtube.com/watch?v=7ySVbKf9vi8
Kuwasilisha Ombi Lako la Kwanza: https://www.youtube.com/watch?v=uW0qlXfU9lQ
Kuwasilisha Ombi Lako la Kila Wiki: https://www.youtube.com/watch?v=tu0M9w-gWS4

Ikiwa huna barua pepe, fungua akaunti ya barua pepe kwenye Gmail (au Yahoo, Outlook).
Ili kufungua akaunti ya mtumiaji mpya katika ReEmployME, tembelea tovuti ya www.maine.gov/reemployme kisha uunde:

**Jina la Kuingia Katika Akaunti: ________________________________________________**

**Nenosiri: ___________________________________________________**

**MUHIMU! Thibitisha anwani yako ya barua pepe baada ya kufungua akaunti yako:**

1. Ukiwa kwenye akaunti yako, nenda kwenye Benefits Maintenance > Update Claimant Profile > Verify E-mail;

2. Kwenye skrini inayofuata, weka Msimbo wako wa Uthibitishaji uliopokewa katika anwani ya barua pepe iliyo kwenye faili ili kuwezesha barua pepe yako, au bofya neno 'here' ili kupata msimbo mpya utakaotumwa katika barua pepe iliyo kwenye faili. (Ikiwa unahitaji msimbo mwingine wa uthibitishaji, bofya 'here'. Utatumiwa barua pepe iliyo na msimbo mpya wa uthibitishaji.)

3. Ikiwa utatumiwa msimbo mpya wa uthibitishaji, rudi kwenye hatua ya 2 iliyo kwenye skrini ile ile kisha weka msimbo ili ukamilishe mchakato wa uwezeshaji.

## Ili kutuma ombi la ukosefu wa ajira, utahitajika kutoa maelezo yafuatayo:


1. Jina la Kisheria (Jina la kwanza, herufi ya kwanza ya jina la katikati, Jina la mwisho)
2. Anwani ya Barua Inayotumika Sasa
3. Nambari Yako Ya Simu
4. Anwani ya Barua Pepe
5. Jinsia (Kiume/Kike)
6. Tarehe ya Kuzaliwa (mwezi, siku, mwaka)
7. Nambari ya Usalama wa Kijamii (SSN)
8. Ikiwa wewe SIO Raia wa Marekani, ni lazima uwe na:
    a. Hali Halali ya Mkazi wa Kudumu (mmiliki wa "Green Card");
    b. Hati ya Idhini ya Ajira ya Marekani ("Kibali cha Kazi"); au

c. Rekodi ya Kuwasili/Kuondoka ambayo inasema "ajira imeidhinishwa" ("I-94 Card").










## Nambari ya Mgeni

- Ukiwa na green card au kibali cha kazi, weka Nambari yako ya Mgeni/USCIS mahali ambapo ombi la mtandaoni linaorodhesha "Alien Number".

- Ukiwa na kadi ya I-94 ya "ajira imeidhinishwa", tafadhali weka nambari yako ya tarakimu 11 ya I-94 mahali ambapo ombi la mtandaoni linaorodhesha "Alien Number".

## Tarehe ya Mwisho ya Hati Yako

Tafadhali weka tarehe ya mwisho ya hati yako iliyo hapo juu.

**KUMBUKA:** Ikiwa hati yako HAINA tarehe ya mwisho, tafadhali weka tarehe ambayo ni mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuwasilisha ombi lako.

- **Mfano:** Ukiwasilisha ombi lako la manufaa tarehe 1/4/2020. Tarehe ya mwisho inapaswa kuwa: 1/4/2021.

## Ustahiki

- Lazima uwe umeruhusiwa kisheria kufanya kazi Marekani katika muda uliopata Mshahara wako wa Kipindi Msingi.
- Lazima uwe umeruhusiwa kisheria kufanya kazi wakati unapodai manufaa ya ukosefu wa ajira.
- Nambari Yako ya Usalama wa Kijamii na/au nambari ya Mgeni itathibitishwa na hifadhidata za shirikisho, kwa hivyo hakikisha umeweka maelezo kamili yanayolingana na hati hizi.

## Maelezo Yanayohitajika ya Mke au Mume na Wategemezi/(watoto)

- Jina la Kisheria (Jina la kwanza, herufi ya kwanza ya jina la katikati, Jina la mwisho**)** la Mke au Mume/Mtoto
- Nambari ya Usalama wa Kijamii
- Uhusiano
- Tarehe ya Kuzaliwa

## Maelezo kuhusu Mwajiri/Historia ya Ajira

<u>Ni lazima uwataje waajiri wako WOTE katika miezi 18 iliyopita ikiwa ulikuwa na ajira zaidi ya moja au waajiiri zaidi ya mmoja</u>

1. Jina la Mwajiri au Waajiri (andika jina kamili la kampuni)
2. Anwani ya Mwajiri au Waajiri (andika anwani kamili ya barua ya kampuni pamoja na msimbo wa

eneo)
    a. Nambari ya Simu ya Mwajiri au Waajiri
    b. Jina la Msimamizi *(halijaulizwa, lakini ni muhimu kujua ikiwa una maswali yoyote)*
3. Nambari ya Mawasiliano au Anwani ya Barua Pepe ya Msimamizi *(halijaulizwa, lakini ni muhimu kujua ikiwa una maswali yoyote)*

## Je, ulifanya kazi hapo kwa muda gani na ulianza lini?

1. Tarehe zako za hivi majuzi za ajira/ulipokuwa ukifanya kazi
    a. Ulianza kazi hii lini? Mwezi, siku, mwaka
    b. Je, uliacha kufanya kazi hii lini (uliachishwa kazi)? Mwezi, siku, mwaka
2. Je, unafanya kazi kwa saa ngapi kila wiki? Kwa muda wote/kwa sehemu ya muda tu?

## Ulilipwa pesa ngapi?

1. Ulilipwa pesa ngapi kwa saa moja? Malipo kwa kila saa?
2. Malipo ya kila wiki kwa jumla (jumla kabla ya ushuru)
3. Malipo ya kila wiki baada ya ushuru (kiasi haswa ulichopokea). (Angali sehemu ya rekodi-baki ya cheki au malipo ili kuthibitisha)
4. **Malipo ya jumla**: ripoti jumla ya mapato yako ya kila wiki ambayo unafanya kazi unapowasilisha madai, na pia kutoripoti malipo (malipo ya kuachishwa kazi, malipo ya wakati wa likizo, bonasi), yanaweza kupelekea uamuzi wa udanganyifu.

## Je, ungependa kulipwa vipi?

Utaulizwa mbinu yako ya malipo unayopendelea: amana ya moja kwa moja kwenye akaunti yako ya kibinafsi ya malipo au akiba katika benki yako au Kadi ya Malipo ya Kielektroniki (EPC). Hii ni Kadi ya Visa kutoka Benki ya Marekani.

### Ikiwa unataka kulipwa kupitia njia ya amana ya moja kwa moja katika benki, utahitaji:

- Jina la Mtu kwenye Akaunti ya Benki
- Jina la benki
- Anwani ya benki
- Nambari ya simu ya benki
- Akaunti ya Malipo au ya Akiba
- Nambari ya Akaunti
- Nambari ya kubaini benki, "routing number" (inaweza kupatikana kwenye cheki)

Ikiwa unataka kulipwa kupitia Kadi ya Malipo ya Kielektroniki (Kadi ya Visa) utatumiwa kadi ya visa. Maagizo ya kutumia kadi yanatolewa pamoja na kadi. Tembelea www.maine.gov/reemployme na ubofye Payment Options chini ya sehemu ya "Learn About" ili kupata maelezo zaidi.

## Kuzingatiwa kwa Ushuru

Utaulizwa ikiwa ungependelea kulipa ushuru wakati wa kwanza kuwasilisha ombi lako la manufaa (*tunapendekeza kwamba ulipe ushuru ikiwa unaweza, ili usilazimike kulipa ushuru baadaye ukipokea malipo yoyote ya ukosefu wa ajira*). 10% imekatwa kwa ushuru wa Shirikisho? 5% imekatwa kwa ushuru wa jimbo?

- Ikiwa kwa sasa unapokea Bima ya Usalama wa Kijamii (SSI) au unapokea msaada wa umma kwa mtoto wako (TANF),**inawezekana** ulipaji ushuru wa moja kwa moja utaondolewa kwako.

**Mara tu utakapowasilisha, utapokea nambari na barua pepe ya uthibitishaji wakati madai yako yamekubaliwa.** Ikiwa hutapokea nambari ya uthibitishaji,

hujakamilisha mchakato wa uwasilishaji wa ombi.

**LAZIMA uwasilishe udhibitisho kila wiki kwamba unataka kudai manufaa ya ukosefu wa ajira. Unaweza kufanya hivi kupitia akaunti yako ya ReEmployME mtandaoni au kwa njia ya simu.**

## REJELEO

**Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Ukosefu wa Ajira:**
https://www.maine.gov/labor/docs/2020/covid19/covidfaqandui.pdf
**Tovuti ya MDOL Kuhusu Ukosefu wa Ajira:** https://www.maine.gov/unemployment/
**Maelezo ya Ukosefu wa Ajira Yanayohusiana na COVID-19:** https://www.maine.gov/labor/covid19/
**Uwasilishaji wa Ombi Mtandaoni:** **www.maine.gov/reemployme**

**Saa za Ofisi ya Huduma za Manufaa:** Jumatatu – Ijumaa, 8:00 a.m. hadi 5:00 p.m.
**Saa za Huduma kwa Wateja:** Jumatatu – Ijumaa, 8:00 a.m. hadi 12:30 p.m.

**Nambari ya Simu ya Huduma kwa Wateja:** 1-800-593-7660
Huduma kwa Wateja Mtandaoni**:** www.maine.gov/labor/contact (bofya kitufe cha unemployment (ukosefu wa ajira))
Pata Kituo cha CareerCenter/Live Chat: https://www.mainecareercenter.gov/locations/index.shtml